

## MWAKA WA LITURUJIA

Mwendo wa vipindi vya liturujia unafanana na ule wa maisha ya binadamu, ambayo yana maadhimisho ya pekee na majira ya kukua na kukomaa kwa utulivu. Vivyo hivyo mwaka wa Kanisa una sikukuu na siku za kawaida, vipindi vya pekee na la. Sehemu muhimu zaidi ya mwaka inategemea Pasaka na Noeli, sherehe kuu mbili zinazoendesha muda mtakatifu wote, ingawa zimo sikukuu nyingine pia.

### KIPINDI CHA MAJILIO

Katika mwaka wa liturujia ya Kanisa la Roma, sherehe ya Noeli inaandaliwa na kipindi cha Majilio ambacho kina mambo mawili: kinakumbusha Mwana wa Mungu alivyotujilia mara ya kwanza, na papo hapo kinatuandaa kumpokea atakapotujilia tena siku ya mwisho. Kufuatana na hayo kina sehemu mbili: hadi tarehe 16 Desemba kinahusu zaidi kurudi kwa Bwana; siku nane za mwisho kinatuelekeza moja kwa moja kuadhimisha kuzaliwa kwake.

Urefu wa Majilio unategemea siku inayoangukia Noeli, kwa kuwa ni lazima yawe na Jumapili nne. Hivyo basi yanaanza kwa Masifu ya Jioni ya kwanza ya Jumapili inayoangukia tarehe 30 Novemba au tarehe ya jirani zaidi; yanakwisha kabla ya Masifu ya Jioni ya kwanza ya Noeli.

Kwa jumla ni kipindi cha toba: rangi yenyewe ni zambarau; haziruhusiwi sherehe za fahari; ala za muziki na maua vinaweza kutumika kwa kiasi tu. Masharti hayo yanalegezwa katika Jumapili ya tatu kwa sababu ya furaha ya kuona tunakaribia sherehe yenyewe.

Sisi binadamu hatuwezi kuishi daima katika hali ileile bila ya matazamio. Hasa kijana anatarajia mambo mapya tena mema. Hivyo tunajitahidi kuyapata. Asiyetazamia chochote amevunjika moyo, hana hamu ya kuishi. Lakini matazamio ya kibinadamu yakimfikia mtu hayamridhishi moja kwa moja. Kristo tu anatimiza hamu zote kwa kumkomboa kutoka unyonge. Majilio yanatukumbusha kila mwaka matarajio ya kweli na hivyo yanaamsha hamu ya kuishi kwa bidii ya kiroho.

Katika kipindi hicho tunaadhimisha tumaini la Israeli lililotimizwa Yesu alipokuja katika unyenyekevu wa umbile letu; pia tunangojea arudi kwa utukufu. Kama alivyotekeleza ahadi mara ya kwanza, atazitekeleza pia mara ya pili, ingawa kwake miaka elfu ni kama siku moja tu. Kati ya majilio hayo mawili, Bwana anatujilia mfululizo kifumbo katika sakramenti (hasa ekaristi) na katika maisha ya kila siku kwa njia ya matukio na watu (hasa maskini). Basi tunapaswa kuwa tayari daima kumpokea ili siku ya mwisho tukamlaki, naye atukaribishe kwenye uzima wa milele. Pia tunapaswa kumuomba aje kutukomboa, yeye aliye tumaini letu.

Katika safari ya Majilio watu watatu wanatuongoza tukutane na Yesu:

1. Isaya nabii wa tumaini, mwenye kipaji cha kutokeza matazamio ya binadamu na kumhakikishia atatimiziwa na Mwokozi.
2. Yohane Mbatizaji, mwenye kuhimiza toba kwa kuwa tunapaswa kupindua maisha yetu ili tukutane vema na Kristo.
3. Maria, bikira aliyekuwa tayari kumpokea Masiya kwa upendo na kushirikiana naye katika kutimiza mpango wa wokovu.

Tukiwafuata hao watatu tunaweza kujipatia maadili yale yanayotuandaa kumpokea Mwokozi anapotujilia, ambayo ndiyo matunda maalumu tunayotarajiwa kuyachuma wakati wa Majilio:

1. Kukesha katika imani, kusali na kutambua ishara za Bwana kutujilia katika nafasi yoyote ya maisha na mwishoni mwa nyakati.
2. Kuongoka kwa kufuata njia nyofu.
3. Kushuhudia furaha inayoletwa na Yesu kwa kuwa na upole na uvumilivu kwa wenzetu, kwa tumaini la kuwa bidii zetu zinawahisha ufalme wa Mungu wenye heri isiyo na mwisho.
4. Kutunza unyenyekevu kwa kufuata mifano ya maskini wa Injili ambao ndio waliompokea Mkombozi.

### KIPINDI CHA NOELI

Watu wote ni wakosefu na kujenga mazingira maovu hata wanayakinai na kutamani wamuone mtu tofauti, yaani mwema na mtakatifu. Pengine wanadhani fulani ni mwema kabisa, kumbe siyo. Haja hiyo inaturudia sisi: kwa nini nisiwe mimi mtu wa namna hiyo? Kwa nini nisianze na moja kama kwa kuzaliwa upya kabla sijawadai wengine? Zaidi tena, haja kuu ya binadamu ni kumuona Mungu mwenyewe: lakini wapi, lini, namna gani?

Kama kawaida, imani na liturujia ya Kikristo zinaitikia haja za binadamu. Kipindi cha Noeli kinatimiza haja tulizozitaja, kwa kuwa anazaliwa mtu mpya kabisa ambaye anatuvutia kwa wema wake na ambaye tukimuona tumemuona Mungu, tena tukimpokea tunazaliwa upya kama wana wa Mungu.

“Leo amezaliwa kwa ajili yenu Mwokozi, ndiye Kristo Bwana”. Tunapoadhimisha Noeli tangazo hilo la malaika kwa wachungaji linatufikia sisi. Si kujidanganya, kana kwamba Yesu angezaliwa leo, wala hatukumbuki tu tukio la zamani, bali fumbo la kuzaliwa Bwana linatufikia leo katika liturujia na kutuletea neema zake. Hivyo tunaweza tukazaliwa upya kwa kushiriki kuzaliwa kwa kichwa chetu.

Liturujia inashangilia hivi, "Lo! Mabadilishano ya ajabu! Mwana wa Mungu anakuwa mtu kusudi mtu awe mwana wa Mungu!". Tena si binadamu tu, bali viumbe vyote vinapata heshima mpya kwa Neno wa milele kujifanya kiumbe.

Katika kipindi kifupi cha Noeli tunaadhimisha miaka yote ya maisha yaliyofichika ya Yesu hadi ubatizo wake, alipokabili utume wake mgumu. Kwanza kwenye sherehe yenyewe tunaadhimisha kuzaliwa kwake katika unyonge wa ubinadamu wetu na katika ufukara wa pango. Sherehe hiyo inachukua siku nane (Oktava) zinazohesabiwa kuwa moja. Katikati inaadhimishwa Familia takatifu kama mazingira ya kufaa kwa kumpokea huyo Mwana na kama kielelezo kwa familia zote za binadamu. Siku ya nane ni pia mwanzo wa mwaka mpya ambao tunaomba uwe na amani. Ndiyo siku ya Yesu kutahiriwa na kupewa jina hilo linaloeleza maana ya yeye kujifanya mtu (נושׁ = Mungu anaokoa). Lakini hasa tunamshangilia Maria mzazi wa Mungu, sifa yake bora iliyompatia fadhili nyingine zote. Inafuata sherehe ya Epifania (Tokeo la Bwana) ambapo mwanga wa Kristo uliwafikia watu wa mataifa (mamajusi). Siku ya mwisho unaadhimishwa Ubatizo wa Bwana.

Baada ya kipindi cha Noeli kuna majuma kadhaa ya kawaida, halafu vinafuatana vipindi vya Kwaresima na Pasaka.

## KIPINDI CHA KWARESIMA

Kwaresima ni kipindi muhimu cha mwaka kinachoandaa Pasaka. Kwaresima yote inaeleweka tu kama maandalizi ya Pasaka, fumbo la kifo na ufufuko wa Bwana ambalo ndilo lengo la maisha yetu yote. Tunapaswa kuishi kwa ajili yake ambaye alikufa akafufuka kwa ajili yetu. Tunapaswa kuishi pamoja naye na ndani yake kwa kuchukua kila siku mwilini mwetu kifo chake ili kushiriki ufufuko wake. Tunapaswa kufia dhambi ili kuishi maisha mapya yaliyojaa upendo kama ya kwake. Kwa ajili hiyo tunapaswa kujikana na kupoteza maisha yetu nyuma yake ili tuyaokoe kweli. Hayo yote yanafanyika kwa njia ya imani, sakramenti na matendo kabla hayajatimia kwa kifo chetu (hasa kifodini) halafu kwa ufufuko wetu.

Kwenye sherehe ya Pasaka tunatakiwa kutimiza hayo yote vizuri iwezekanavyo: ndiyo maana wakatekumeni watakaobatizwa usiku wa ufufuko, nasi sote tutakaomla pamoja nao Mwanakondoo aliyechinjwa, tunajiandaa kwa bidii za pekee katika kulisha imani yetu kwa Neno la Mungu, katika kushiriki ibada na katika kutekeleza toba. Hivyo kwa pamoja, ingawa kwa namna tofauti, tunapanda Yerusalemu pamoja na Yesu na wanafunzi wake wote kwa ajili ya Pasaka.

Ni kawaida ya binadamu katika shughuli yoyote kufikia hatua ya kuona haja ya marekebisho, ya hali mpya, hasa mbele ya maonevu na utumwa. Katika historia mara nyingi walijitokeza watu waliohisi sana haja hiyo na kuelekeza njia ya ukombozi. Kwa Wakristo safari hiyo inafanyika hasa wakati wa Kwaresima kwa kuzingatia uharibifu uliotokana na dhambi katika maisha yao binafsi na katika jamii. Wakiongozwa na Yesu wanajitahidi kurekebisha uhusiano wao na Mungu, na watu na vitu ili kuanza na moja maisha adili.

Katika Agano la Kale Musa ndiye aliyepanga Waisraeli. Sisi tunakumbuka na kufuata safari yao ya ukombozi, walipokaa jangwani miaka 40 ili kuelimishwa kinaganaga juu ya yale yatokanayo na maneno ambayo Musa alipewa na Mungu alipofunga siku 40 juu ya mlima Sinai. Hayo yalikamilishwa na Yesu katika Agano Jipya: ndiye kiongozi na mkombozi wetu na wa wote. Kabla hajaanza utume wake, yeye pia alifunga siku 40 jangwani akijilisha matakwa ya Baba ili ayatekeleze na kuwatangazia watu wote.

Kufuatana na hayo yote Kanisa linafunga siku 40 katika jangwa la kiroho. Wakati wa Kwaresima linatuongoza katika safari ya kujirekebisha kulingana na Neno la Mungu la Agano la Kale na la Agano Jipya. Wote tunahimizwa kufunga safari hiyo kadiri ya hali yetu: kwanza wale wanaoijiandaa kubatizwa usiku wa Pasaka (hasa kwa kufanyiwa mazinguo matatu yanayofuatana katika Dominika III, IV na V), lakini pia sisi tuliokwishabatizwa, ambao kabla ya hapo tunatakiwa kutubu na kuungama dhambi zetu ili turudie kwa unyofu ahadi za ubatizo. Makundi yote mawili tutakula pamoja Mwanakondoo ili tuishi upya kwa upendo, jambo litakalofanya hata wasio Wakristo wafurahie Pasaka.

Kazi za urekebisho zinahitaji juhudi za pekee. Vivyo hivyo kwa ukombozi wa kiroho Kwaresima inadai bidii nyingi pande mbalimbali: katika kufunga, kutoa sadaka, kusali na kusikiliza Neno la Mungu hasa wakati wa ibada. Hayo yote yanahusiana na kusaidiana.

Mkristo akijinyima chakula cha mwili anajifunza kufurahia zaidi mkate wa Neno la Mungu na wa ekaristi, tena anatambua zaidi anavyopaswa kuwahurumia wenye njaa na shida mbalimbali. Toba inahimizwa isiwe ya ndani na ya binafsi tu, bali pia ya nje na ya kijamii: itokane na upendo na kulenga upendo kwa kurekebisha kasoro upande wa Mungu (sala), wa jirani (sadaka) na wa nafsi yetu (mfungo).

Mfungo, yaani kujinyima tunavyovipenda na hata tunavyovihitaji, uwe ishara ya njaa yetu ya Neno la Mungu, ya nia yetu ya kushiriki mateso ya Yesu yanayoendelea katika maskini, ya kulipa kwa dhambi zetu na kuachana nazo. Sadaka inayotokana na sisi kujinyima inampendeza Mungu kuliko ile isiyotuumiza; msaada unaweza kutolewa pia kwa kutetea haki za binadamu dhidi ya wanyanyasaji. Sala inastawi kwa kusikiliza sana Neno la Mungu hasa kwa pamoja (katika familia, jumua, liturujia n.k.). Ndiyo maana wakati wa Kwaresima Kanisa linazidisha nafasi za kulitangaza na hivyo kuelimisha wote kuhusu mambo makuu ya imani na maadili yetu.

Kuna mpangilio kabambe wa masomo ya Misa, hasa ya Dominika, ili wote wafuate hatua kuu za historia ya wokovu (somo la kwanza) na kuchimba ukweli wa ubatizo (mwaka A), agano na fumbo la Kristo (mwaka B) na upatanisho (mwaka C). Kwa njia hiyo tunatangaziwa jinsi Mungu anavyotuoakoa; pia

upande wetu kuanzia Dominika ya kwanza tunajielewa kuwa watu vishawishini ambao tunapaswa kushinda kwa kumfuata Yesu, si Adamu: kwenda jangwani ili kumtafuta Bwana na matakwa yake. Kilele cha safari ya Kwaresima ni Dominika ya Matawi, tunapoingia Yerusalemu pamoja na Yesu anayekwenda kufa na kufufuka kwa ajili yetu. Liturujia ya siku hiyo ina mambo mawili: kwanza shangwe (katika maandamano), halafu huzuni (kuanzia masomo, ambayo kilele chake ni Injili ya Mateso). Baada ya Kwaresima kwisha, tutapitia tena historia ya wokovu katika kesho la Pasaka ambapo hatua zote zinaangazwa na ushindi wa Kristo mfufuka.

## SIKU TATU KUU ZA PASAKA

Bawaba inayoviunganisha vipindi vya Kwaresima na Pasaka ni siku tatu kuu za Bwana mteswa (kuanzia Alhamisi Kuu jioni hadi Ijumaa Kuu jioni), mzikwa (kuanzia Ijumaa Kuu jioni hadi Jumamosi Kuu jioni) na mfufuka (kuanzia Jumamosi Kuu jioni hadi Jumapili ya Pasaka jioni). Ibada za siku hizo ni za pekee: hivyo ni lazima ziandaliwe vizuri pamoja na watu wa kutosha. Haziruhusiwi nyimbo za kawaida, na vilevile zile za pekee za siku hizo hazitakiwi kuimbwa nyakati nyingine za mwaka.

Alhamisi Kuu jioni tunaadhimisha mambo matatu yaliyowekwa na Yesu katika karamu ya mwisho: ekaristi, upadri na amri mpya. Siku hiyo yeye alifanya kiibada kile atakachofanya kihistoria katika Pasaka yake, akatuagiza tufanye daima kwa ukumbusho wake. Nasi tunatekeleza agizo hilo kwa namna ya pekee siku yenyewe, tukijisikia tupu naye mezani. Kila mahali Misa iwe moja; Askofu tu anaweza kuruhusu nyingine kwa wale wasioweza kuihudhuria. Padri hawezi kuadhimisha Misa peke yake kwa sababu hiyo ni siku ya umoja. Tabenakulo iwe tupu, kwa kuwa ndiyo siku ya ekaristi kuwekwa na Yesu. Misa inaanza kwa furaha: tunaweza kugonga kengele, ila wakati wa kuimba Utukufu ndiyo mara ya mwisho mpaka kwenye Utukufu wa usiku wa Pasaka. Ni vema mwanzoni mwa Misa hiyo kupokea kwa shangwe krisma iliyowekwa wakfu na mafuta matakatifu yaliyobarikiwa asubuhi (au siku nyingine ya jirani) katika Misa ya Krisma, ambapo mapadri walirudia ahadi zao mbele ya Askofu. Jambo lingine la pekee ni padri kutawadha miguu ya wanaume 12 kama ukumbusho wa tendo la Yesu kwa mitume wake, ambalo alituelekeza kutumikia kwa upendo mnyenyekevu. Kwa matoleo kuna wimbo maalumu wa Mt. Paulino wa Aquileia ("Palipo na Upendo na Mapendo"). Inafaa wakati wa komunyo mashemasi na wengineo wapeleke ekaristi kwa wagonjwa. Baada ya komunyo kuna maandamano ya kuiweka sakramenti kwa ajili ya kesho yake ambayo haitakuwa na Misa (wimbo maalumu, uliotungwa na Mt. Thoma wa Akwino, ni "Sakramenti Kubwa Hiyo"). Tunahimizwa kuiabudu ekaristi huku tukisoma maneno aliyotamka Yesu usiku huo kabla hajakamatwa (Yohane 13-17); baada ya saa 6 usiku kusiwe na fahari wala shangwe.

Ni lazima kufunga chakula na kujinyima nyama Ijumaa Kuu na ikiwezekana Jumamosi Kuu pia. Siku hizo mbili hakuna Misa, ila ni desturi kuadhimisha pamoja na walei Ofisyo ya Giza (Kipindi cha Masomo na Masifu ya Asubuhi) ili kuzidi kutafakari.

Pia Ijumaa Kuu alasiri kuna Ibada ya Kifo cha Bwana, ambayo ina sehemu tatu: liturujia ya Neno, kuabudu msalaba na komunyo: tunaweza kupokea ekaristi iliyobaki jana yake, lakini si katika umbo la divai, iliyo ishara ya furaha. Siku hiyo sakramenti nyingine haziruhusiwi isipokuwa kitubio, mpako wa wagonjwa na ubatizo katika hatari. Altare iwe tupu. Padri na watumishi wanapoingia hakuna wimbo wowote. Wakishafika mbele ya altare wanajilaza kifudufudi kama kwa kuishiwa nguvu mbele ya fumbo la mateso ya Bwana, huku waamini wakipiga magoti kimya kabisa. Mara baada ya hapo padri anaanza sala bila ya utangulizi. Yanafuata masomo (bila ya kuyapunguza) ambayo kilele chake ni Mateso kadiri ya Yohane. Baadaye yanafanyika kwa urefu mkubwa, kama yalivyokuwa zamani, maombi (kwa kawaida 10) yanayokumbatia watu wote, kwa kuwa ndiyo siku ya Yesu kujitoka kwa ajili ya wote. Katika sehemu ya pili tunaabudu si mti, bali fumbo la msalaba. Kanisa linataka daima ishara zote ziwe za kweli, hivyo haliruhusu maua ya karatasi au plastiki wala mishumaa ya umeme. La sivyo hata matendo na maneno yetu katika ibada hayatakuwa na maana halisi: yatafanana na yale ya Yuda alipombusu Yesu kwa kumsaliti. Basi, ishara yake iwe msalaba mmoja na mkubwa wa kutosha, si mingimingi midogo, kwa sababu aliyekufa kwa ajili ya wote ni mmoja tu. Watu wakiwa wengi mno, baada ya baadhi yao kuabudu msalaba binafsi (k.mf. kwa kuubusu), padri anaweza kuinua ili waliobaki wauabudu kwa pamoja (k.mf. kwa kuupigia magoti). Baadaye altare inavikwa na hostie zilizobakizwa jana zinaletwa ili kuwagawia watu, lakini zikibaki tena ni lazima zipelekwe nje ya kanisa, ili tuonje hali ya ukiwa kama ile ilivyowapata mitume: tumeondolewa Bwanaarusi. Kanisa linakumbuka lilivyozaliwa kama Eva Mpya kutoka ubavu wa Adamu Mpya aliyetokwa na damu na maji, ishara za sakramenti zake. Altare inavuliwa tena, kwa sababu haitakiwi kutumika. Tukipita mbele ya msalaba tunapiga goti hadi Jumamosi Kuu jioni.

Jumamosi Kuu kwa jumla ni siku ya kimya na kutafakari. Zinaweza kutumika picha za Yesu msalabani, kaburini au kuzimu; pia picha za Bikira Maria wa mateso.

Ibada kuu kuliko zote ni ile ya usiku wa Pasaka (isiitwe Misa ya Jumamosi Kuu!). Ni lazima ifanyike yote usiku tu: ianze baada ya jua kutua na iishe kabla halijapambazuka. Kama Yesu alivyofanya, Kanisa linaagiza tukeshe daima. Kati ya makesha yote, lile la usiku wa Pasaka linaitwa mama wa makesha: ni kumkaribisha Yesu mshindi arudi ulimwenguni. Mpangilio wa kesho una sehemu nne: liturujia ya mwanga (inayotuingiza katika fumbo la ufufuko), liturujia ya Neno (kwa kawaida ina masomo 9), liturujia ya ubatizo (ambao unaadhimishwa, hasa kwa watu wazima, au walau unakumbukwa) na liturujia ya ekaristi (ambapo tunakutana kwa namna mpya na Yesu mfufuka). Uzito wa sehemu ya mwanga uko hasa katika

ishara (moto mpya, ubani, mshumaa wa Pasaka, mishumaa ya kila mwamini n.k.) na vitendo vyake ambavyo vifanyike kwa heshima ya pekee (kutembea nyuma ya mshumaa mkuu wa Yesu mfufuka kama Waisraeli walivyofuata mnara wa moto jangwani, kuwasha mishumaa yetu, kuangaza Kanisa lote n.k.). Kilele chake ni mbiu ya Pasaka inayoimbwa kwa fahari sana. Baada ya hapo tunazima mishumaa yetu mpaka tutakapoiwasha tena ili tuuungame imani pamoja na kurudia ahadi za ubatizo. Sehemu kubwa ya kesho inachukuliwa na masomo 7 ya Agano la Kale ambayo kila moja linafuatwa na wimbo na sala vinavyotusaidia kuelewa kadiri ya adhimisho na maisha. Kwa wimbo wa Utukufu tunaingia katika Misa na shangwe zinazidi hadi Aleluya inapoanza kuimbwa upya baada ya Kwaresima nzima. Baada ya Injili na hotuba, ungamo la imani linafanyika kuhusiana na ubatizo.

Katika Misa ya mchana, inafaa kutumia maji yaliyobarikiwa usiku ili kukumbuka vilevile ubatizo wetu uliotushirikisha ushindi wa Yesu. Jambo lingine la pekee ni sekwenya ya lazima baada ya somo la pili.

## KIPINDI CHA PASAKA

Wayahudi waliadhimisha Pasaka ya kale, ukumbusho wa kuvuka pakavu kati ya bahari, kutoka utumwani kuelekea uhuru. Sisi tunaadhimisha Pasaka mpya, ukumbusho wa sadaka ya Agano Jipya la milele ambayo pamoja na Yesu tunavuka toka dunia hii kwenda kwa Baba: Kristo asingefufuka imani yetu ingekuwa bure. Wakati wa Pasaka hatusomi Agano la Kale kwa kuwa yaliyotabiriwa nalo yameshatimia katika Kristo. Badala yake tunasoma karibu mfululizo Matendo ya Mitume yanayoelekeza safari yote ya Kanisa. Masomo mengine, sala na nyimbo vinasema hasa juu ya Kristo kufufuka na kuwa nasi na juu ya paji la Roho Mtakatifu alilotupatia.

Katika maisha ya kawaida watu wanafanya sherehe mbalimbali, si za dini tu. Sikukuu yoyote inatokeza furaha ya kuishi: usipokuwa na mtazamo wa kuridhika na maisha, kumwaga pesa katika anasa hakuondoi huzuni ya kukata tamaa. Sikukuu yoyote ni adhimisho la pamoja: inatokana na watu kukubaliana katika kujali mambo fulanifulani au walau kuheshimiana; pia inajenga jamii kwa kurudisha furaha ya kuwa pamoja.

Kwa Wakristo sherehe kuu kuliko zote ni Pasaka: ndiyo sikukuu yenyewe ambayo inadumu siku hamsini mfululizo hadi Pentekoste na inaitwa Dominika kubwa. Kwa kweli Pasaka si sherehe mojawapo tu wala kipindi kimojawapo tu katika mwaka wa liturujia, bali ndiyo kiini chake, kama vile Dominika (Pasaka ndogo ya kila wiki) ilivyo kiini cha juma zima. Ni adhimisho la uzima mpya na wa milele aliotushirikisha Kristo mfufuka kwa njia ya sakramenti: ubatizo na kipaimara kwa Wakristo wachanga, kitubio kwa waliobatizwa zamani, hasa ekaristi kwa wote; humo hatumkumbuki tu Yesu, bali tunakutana naye, hai tena mtukufu. Adhimisho hilo ni la pamoja kwa sababu tumekuwa moyo mmoja na roho moja katika Kristo kwa kumiminiwa Roho Mtakatifu. Kwa kumega mkate mmoja tunaimarisha ushirika wetu na kuwajibika kumtambua Yesu katika wale wote tunaokutana nao, hasa maskini.

Mang'amuzi hayo ya imani yanatuchoea kuimba mfululizo, Aleluya! Bila ya shaka tunaimba tukiwa njiani kuelekea kwetu: hatujafikia pale tutakapoimba katika heri ya starehe ya milele. Tunaimba tusije tukalemewa na mzigo wetu wa maisha. Mt. Augustino anatuonya: "Imba anavyofanya msafiri. Imba lakini tembea, usahau uchovu wako kwa kuimba, lakini jihadhari na uvivu. Imba na tembea". Aleluya inatokeza vizuri furaha na tumaini letu: ndiyo sababu tunaikariri sana. Pamoja na hayo, uhuru wetu unatudai tuushuhudie kwa matendo na hasa kwa kuwakomboa ndugu zetu wanaodhulumiwa.

Kristo amefufuka kweli na atatufufua sisi pia: tutaishi naye kwa Baba katika umoja wa Roho Mtakatifu. Hata sasa yu pamoja nasi (ndiyo maana ya mshumaa wa Pasaka). Tukiwa naye maisha yanatunogea, kwa kuwa yote yameinuliwa tena na kufanywa mapya. Tumekombolewa kutoka utumwa wa dhambi na mauti, tumekuwa wana wa Mungu na kuishi kwa uhuru wa upendo tukiongozwa na Roho Mtakatifu. Kristo amekuwa Bwana na anaendelea kueneza ufalme wake. Hatuwezi kuogopa chochote tena kwa kuwa historia ni yake yeye aliye Alfa na Omega.

## KIPINDI CHA KAWAIDA

Baada ya kila mfululizo wa vipindi viwili vya pekee (Majilio na Noeli, Kwaresima na Pasaka), tunarudia Kipindi cha Kawaida, kinachochukua muda mrefu kuliko vingine vyote pamoja. Hapo sherehe kuu hizo zinapisha maadhimisho manyofu lakini motomoto: ndio wakati murua wa kung'amua upya utajiri wote wa Dominika kama siku ya kukutana na Bwana mfufuka kila wiki ili kwenda ulimwenguni kote kutangaza ushindi wake; kama siku ambayo inaendesha mwaka mzima ikitukumbusha kwa nguvu tunavyohitaji uwiano mzuri wa kazi na pumziko; kama siku inayodai tusimamisha shughuli zetu nyingi za kujitafutia mapato ili kupata nafasi ya kuadhimisha bure upendo wa Mungu anayetuokoa; kama siku inayokumbusha mwanzo wa uumbaji wa ulimwengu, mwanzo wa uumbaji mpya katika ufufuko wa Yesu na hatua nyingine ya safari yetu duniani.

Ekaristi ya Dominika ndiyo chakula cha safari hiyo kinachotutia nguvu mpya daima tuzidi kumuelea Bwana. Katika kutimiza agizo lake la kufanya ukumbusho wake, tunapokea upya toleo kamili la nafsi yake na tunakubali kujitoa kama alivyojitoa kwetu kwa upendo upeo. Si amri ya Kanisa tu, bali ni haja ya moyo wetu. Ndiyo sababu mwaka 304 wafiadini wa Abitene walikiri mbele ya watesi wao: "Hatuwezi kuishi bila ya Siku ya Bwana". Ni siku ya Kanisa, yaani mkusanyiko: viungo vyake vikikutana, mwili huo wa Bwana

unatimia na kudhihirika mbele ya wote. Ni siku ya furaha na amani ambayo inaambukiza kuanzia yeye na inazidi kutufanya ndugu.

Ikiwa vipindi vya pekee vya mwaka vinaadhimisha matukio makuu ya Kristo, hiki cha kawaida kinaadhimisha ushiriki wetu katika fumbo lake ndani ya Kanisa kwa njia ya Roho Mtakatifu. Kristo ameshatimiza kazi ya ukombozi, lakini upande mwingine mambo bado, hadi huo ufafikie watu wote, na kila mmoja apate kuwa mwana huru wa Mungu ndani ya Kanisa, mwili wa Kristo unaoendelea kuishi na kutenda ulimwenguni karne hadi karne. Moyo wa Yesu unazidi kudunda katika kifua cha Kanisa, ambalo ni Kristo ndani yetu, anayezidi kuenea duniani kote. Humo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu neno lake linazidi kuwa hai na kupiga mbio, huku Kanisa likilifanua na kulitekeleza katika mazingira mapya daima.

Kanisa linaalika wanae wakomae katika maisha ya Kiroho kwa kushuka vilele vya Pasaka na Noeli ili kufaidika na malisho mapana ya Kipindi cha Kawaida kwa kutafakari katika mwanga wa ufufuko wake yale yote aliyoyasema na wa kutekeleza yale yote yaliyoyaagiza. Kuadhimisha na kuishi fumbo la Kristo katika hali ya kawaida ni kukubali uwajibikaji mwaminifu wa kila siku ili kumtambua kama Mwalimu anayeongozana nasi katika safari ya maisha, na hivyo kung'amua kwamba Mungu anatuinamia na kutuokoa katika maisha yetu ya kila siku. Ndiyo sababu kipindi hicho kinakazia pia utume wa Kiinjili wa Kanisa ulimwenguni na wajibu wa kuutumiza.

Kipindi hiki ni cha kawaida kwa maana kinaadhimisha fumbo la Kristo kwa jumla, kufuatana na Dominika na siku nyingine za wiki. Kwa ajili hiyo tunasaidiwa na somo la karibu mfululizo la mojawapo kati ya Injili Ndugu ili kutafakari maisha na mafundisho ya Yesu kadiri ya Yesu mwinjili (kwa zamu: Marko, Mathayo halafu Luka siku za kazi; Mathayo mwaka A, Marko mwaka B na Luka mwaka C siku za Jumapili). Humo, mbali na mafumbo makuu tuliyoadhimisha katika vipindi vya pekee vya mwaka wa Kanisa, tunakutana na Yesu katika maneno na matendo yake ya kawaida zaidi, katika mafungamano yake na watu, kuanzia urafiki na wanafunzi wake hadi malezi kwa watu wote. Lengo si tu kukumbuka alivyofanya wakati ule, bali hasa kutambua anavyozidi kufanya kila leo kupitia Kanisa lake.

Kwa Kiingereza, kipindi hicho kinaitwa "Ordinary Time", yaani "muda ambao unafuata utaratibu", hivyo unalingana kabisa na mpango wa upendo wa Mungu na unaleta amani, ambao ni "utulivu wa utaratibu" (Mt. Thoma wa Akwino). Muda huo una pande mbili: kuanzia siku inayofuata Ubatizo wa Bwana hadi siku inayotangulia Jumatano ya Majivu, halafu kuanzia Jumatatu baada ya Pentekoste hadi mchana wa Jumamosi ya tarehe yanapoanza kuadhimishwa Majilio. Katikati ya hizo sehemu mbili za kipindi cha kawaida, mfululizo wa Pasaka unaadhimisha yale Yesu aliyoyafanya katika maisha yake ya hadhara (Kwaresima: kuanzia vishawishi jangwani hadi kifo msalabani) na ushindi wake kamili (Pasaka: kufufuka, kupaa na kumtuma Roho Mtakatifu).

Kwa Kilatini siku ya kazi inaitwa na Kanisa "feria" (wingi wake unamaanisha likizo, starehe), kwa sababu kwa Mkristo kila siku ni sikukuu. Hivyo hata Kipindi cha Kawaida ni cha pekee, kwa kuwa maisha yake yamegeuzwa na kufichika pamoja na Kristo ndani ya Mungu. Kwa mtazamo wa imani hata muda wa kawaida unaweza ukawa na utajiri mkubwa ajabu.

Mapokeo ya Roma yanaadhimisha wakati huo sherehe kadhaa (Utatu Mtakatifu, Mwili na Damu ya Kristo, Moyo Mtakatifu wa Yesu), lakini hizo haziadhimishi tukio fulani, bali ukweli uliobainishwa na mitaguso mikuu kuhusu nafsi tatu za Kimungu, uwepo wa Yesu katika Kanisa kupitia maumbo ya mkate na divai, upendo wake unaowakilishwa na moyo uliotobolewa ili utokwe na chemchemi za neema zinazosababisha Kanisa lizaliwe na sakramenti. Dominika ya mwisho inamshangilia Kristo kama Mfalme wa ulimwengu atakavyodhihirika siku ya kiyama, na hivyo inaturudisha kwenye mada ya kwanza ya Majilio, mwanzo wa mwaka mpya wa Kanisa.

Pia sikukuu nyingi za watakatifu zinapatikana wakati huo, bila ya kuzuiwa na vipindi vya pekee: k.mf. Yohane Mbatizaji, Petro na Paulo, Malaika Wakuu, na hasa Mama Maria. Hata ndani mwao tunazidi kumuadhimisha Kristo, kwa kuwa ni mashahidi wa ushindi wake dhidi ya dhambi na ni ufafanuzi hai wa utakatifu wake unaoendelea kudhihirika ndani ya Kanisa linalohuishwa na Roho Mtakatifu.

Mwishoni mwa kipindi hicho, mwezi Novemba unaadhimishwa Kanisa Shindi la mbinguni (tarehe 1), Kanisa Toharani (tarehe 2) na Kanisa Safiri duniani (tarehe 9). Ni kwamba katika wiki 33 au 34 za Kipindi cha Kawaida (kati yake 5 hadi 9 zinatangulia Kwaresima, halafu 23 hadi 28 zinafuata Pentekoste), Kanisa likihiji kati ya dhuluma za ulimwengu na faraja za Mungu, linazidi kutangaza mateso na mauti ya Bwana mpaka arudi, likielekea uzima wa milele. Wakati huo ufalme wa Mungu unazidi kujengeka na kukua taratibu kuelekea utimilifu wake. Ndiyo maana rangi ni ya kijani, ambayo tangu zamani inahusishwa na uzima mpya na ustawi. Katika Kiebrania jina la rangi hiyo lina maana ya "kijana" pia. Katika Ukristo, rangi hiyo inamaanisha uzima mpya unaotumainiwa katika ufufuko na ule wa Kanisa baada ya Roho Mtakatifu kulijaza Pentekoste ili azidi kummwilisha Kristo katika viungo vyake.